KAMUSI YA SEMI:
Maana na Matumizi

Abel Mkota
na
Fauzia Sakara

Vide~Muwa Publishers Limited
An eye for quality

Kamusi ya Semi: Maana na Matumizi
Kitabu hiki kimetolewa kwa mara ya kwanza 2011
na Vide~Muwa Publishers Limited
S.L.P. 3839-00506 Nairobi, Kenya
Barua pepe: enquiries@vide-muwapublishers.com

© Abel Mkota, Fauzia Sakara, 2011

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote bila idhini, kwa maandishi, ya Vide~Muwa Publishers Limited.

Chapa ya Kwanza, 2011

Usanii na Uandalizi wa:
Jalada: Co-Edit Tools, Nairobi, Kenya.
Matini: Vide~Muwa Publishers Ltd.

ISBN 9966-773-61-4

Kimepigwa chapa na Printing Services
S.L.P. 32197 -000600,
Nairobi Kenya.

PL8703
.M56
2011

Dibaji

Lugha ya Kiswahili, kama lugha yoyote nyingine ile, ni lugha yenye utajiri mkubwa wa misemo na semi. Utajiri huu ni hazina kubwa kwa msomaji na mwanafunzi anayejifundisha lugha hii. Mwanafunzi na msomaji anayeimudu fani ya semi huwa mdarisi mzuri wa lugha hii na huonewa fahari na wasikilizaji wake.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuutambua utajiri huo na kwa nia ya kumsaidia mwanafunzi, mwalimu na mpenzi wa lugha ya Kiswahili kujua maana na matumizi ya misemo na semi hizo tofauti pamoja na kuyamudu matumizi ya fani hii ya semi.

Ingawa wapo wataalamu wanaotumia neno 'misemo' na 'nahau' kujumlisha tungo zinazozungumziwa hapa, tumechagua kutumia neno 'semi' kujumlisha tungo ambazo si methali, vitendawili au tashbihi ambazo hutumiwa kuelezea hali fulani kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Neno hili 'semi' limetumiwa hapa kwa maana yake finyu wala si maana iliyoko katika fasihi simulizi ambayo inajumlisha methali na vipera vingine.

Kamusi ya Semi: Maana na Matumizi imetumia utaratibu sawa na *Kamusi ya Methali: Maana na Matumizi*. Semi inayohusika imefafanuliwa kuanzia maneno yake yasiyokuwa mepesi au ya kawaida (msamiati wake), maana yake na hatimaye mifano ya jinsi ya kuitumia kutolewa. Zipo semi ambazo huwa na maana zaidi ya moja. Hali hii imeonyeshwa kwa matumizi ya tarakimu (1, 2) na hatimaye mifano nayo kutumia mkumbo huo ili kumsaidia mtumiaji wa kitabu chenyewe.

Mpangilio uliotumiwa katika *Kamusi ya Methali: Maana na Matumizi*, wa kuorodhesha visawe vya methali umetumiwa hapa pia. Visawe vinavyotolewa ni vibadala au jinsi nyingine ya kuisema semi inayohusika. Neno 'kisawe' halikutumiwa kwa maana ya semi zenye maana sawa na semi inayohusika bali ni jinsi nyingine ya kuieleza semi fulani – yaani ni muundo mwingine wa semi hiyo hiyo. Tuangalie mfano ufuatao:

ona takilifa. Ni semi yenye maana ya kukumbana na matatizo au shida. Kisawe ni: ona taklifu. Yaani badala ya kusema 'ona takilifa' mtu anaweza kusema 'ona taklifu'. Hata hivyo, kuna semi nyingi ambazo zina maana sawa na ona takilifa kama:

1. kula mumbi.
2. meza mrututu.
3. ona cha mtema kuni.

Utaratibu huu wa kutumia kisawe kwa maana ya jinsi nyingine ya kuisema semi umetumiwa ili kuondoa mtindo wa kupigia mstari au kusema pia. Pili, kwa kutoweka pamoja semi nyingine zenye maana sawa kama kisawe, kitabu kimehakikisha kuwa semi hizo nyingine zimeelezwa kwa ukamilifu na maneno yake yasiyokuwa ya kawaida kuelezwa ipasavyo.

Sifa nyingine ambayo inaonekana hapa ni kufafanua maana ya maneno yaliyotumiwa katika semi tofauti. Ufafanuzi au maelezo ya maana yamefanywa ili kuirahisisha kazi ya msomaji. Hapa tumemuwazia msomaji ambaye hana ujuzi wa kutosha wa lugha ya Kiswahili – ambaye anaweza kuelewa maana ya maneno bila ya kuangalia kamusi za lugha.

Semi za Kiswahili ni nyingi sana. Semi hizi hupatikana kwa mapana na huwa na unyumbufu mkubwa zinapolinganishwa na methali. Semi huundwa kila wakati na wazungumzaji wa lugha yoyote. Hata hivyo, si semi zote ambazo mwishowe huimarika kimatumizi. Kuna nyinginezo ambazo hupotea baada ya kipindi kifupi cha matumizi. Katika uandishi wa kitabu hiki, tumejifunga kwa semi zile tu ambazo zimeimarika katika matumizi.

Hii haina maana kuwa semi zote za Kiswahili zinapatikana hapa. La. Hakuna kamusi inayoweza kudai kuwa imekamilika kwa upande huo. Na kama ingewezekana kukamilika, basi vitabu visingekuwa na matoleo mengine. Pili, lugha huendelea kukua kadiri inavyotumiwa na wazungumzaji wake. Ukuaji huo unatokea pia katika medani ya semi na nahau: huzuka nahau na semi mpya na nyingine zilizotumiwa kwa miaka mingi zikafifia na kutoweka kabisa.

Ni matumaini yetu kuwa watumiaji wa kamusi hii, nchini Kenya, Tanzania, Uganda na kwingineko kinakotumiwa Kiswahili, watafaidika na kamusi hii na kwamba itakuwa kanzi muhimu itakayowasaidia kuimudu fani hii muhimu ya lugha ya Kiswahili.

Abel Mkota na Fauzia Sakara,
Novemba - Desemba 2009.

Aa

-a kufa mtu.

Maana: kali sana, -enye udhati mkubwa.

Matumizi: Itabidi ziwepo juhudi *za kufa mtu* ili tufanikiwe katika kazi inayotukabili.

-a kufutia machozi.

Maana: kitu cha kujifariji au kujituliza baada ya hali kwenda vibaya (aghalabu katika mchezo).

Matumizi: Timu ya Kilimanjaro Stars ilifunga magoli manne katika kipindi cha kwanza lakini mshambulizi wa timu ya Uganda Cranes aliwafungia goli moja *la kufutia machozi* katika kipindi cha pili.

-a ndani.

Maana: Hutumiwa kuelezea jambo la siri; la moyoni au linalomhusu mtu fulani.

Matumizi: Haifai kuyafichua mambo *ya ndani* kati yako na jamaa yako mbele za watu.

-a nguvu.

Maana: -a thamani au muhimu; yenye thamani kubwa; maarufu.

Matumizi: Maria ameolewa na mfanyabiashara *wa nguvu* wa mjini.

abadan kataan.

Maana: m.s. *abadan* ni kamwe; asilan. Pia abadani. *Kataan* ni neno la kusisitiza kinyume. Msemo huu hutumiwa kusisitiza kutotokea kwa jambo.

Matumizi: Mkurugenzi amesema hawezi *abadan kataan* kukubali shirika liende hasara ili kuwaridhisha wachache.

acha kitu mnofu nyuma.

Maana: m.s. *mnofu* ni kipande cha nyama aghalabu kisichokuwa na mfupa wowote. Msemo huu hutumiwa kuelezea hali ya mtu kuacha kitu au mali inayoonyesha kuwa aliwahi kuwa na utajiri au uwezo fulani.

Matumizi: Yule mfanyabiashara amefariki bila *kuacha kitu mnofu nyuma* cha kuonyesha utajiri wake.

acha kujenga nyumba ya karata.

Maana: Nyumba zinazojengwa kwa karata huanguka haraka sana. Msemo huu hutumiwa kumnasihi mtu asiwe na ndoto zisizokuwa na msingi wowote.

Matumizi: Mbunge yule anapaswa *kuacha kujenga nyumba za karata* kwa kudhani anaweza kupigiwa kura kama rais wa nchi hii.

acha maagizo.

Maana: m.s. *agizo* (wingi: maagizo) ni amri ya kufanya au kutenda jambo fulani. Toa maagizo ya kutenda jambo hasa mtu anapoondoka.

Matumizi: Mama *ameacha maagizo* kwa mlezi wa mtoto kumlisha mtoto vizuri.

acha mavanga.

Maana: m.s. *mavanga* ni uongo; hadaa au madanganyo. Epukana na uongo au udanganyifu.

Matumizi: *Usipoacha mavanga* utaishia kujuta siku moja uongo wako utakapogunduliwa na kila mtu.

acha mizengwe.

Maana: acha maneno ya kuzungushazungusha; acha mambo yasiyoeleweka.

Matumizi: Ukitaka ueleweke na wenzako lazima uzungumze